**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI KWA OFISI YA RAIS IKULU KUPITIA RIPOTI YA KAMATI YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia Uhai na Afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu. Vile vile, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wako kwa kuliongoza vyema Baraza hili Tukufu kwa umahiri mkubwa na ninaamini kwamba mtaendelea kuliongoza kwa uadilifu wa hali ya juu zaidi ili kufikia malengo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020 -2025 pamoja na Mipango na Mikakati mbali mbali ya Kitaifa katika kufikia hatua iliyobora kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia, kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake uliotukuka ambapo ndani ya muda mfupi tu wa miaka miwili tumeona mambo aliyowafanyia wananchi wetu na kila mmoja ni shahidi katika mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii. Kamati inaridhika sana na juhudi za Mheshimiwa Rais za kutembelea maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kutatua matatizo ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, uadilifu anaotuonesha unapelekea kupatikana kwa maendeleo ya kudumu mbali mbali kwa msingi ule ule wa kudumisha amani na utulivu wa Taifa hili. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa hekma, busara na nguvu katika utumishi wake. Kwa hakika Kamati yetu imeridhika sana na uongozi wake pamoja na kwamba dunia imekuwa ikikabiliwa na majanga ya maradhi ya Korona na Vita vya Urusi na Ukrain hali ambayo imesababisha kuporomoka kwa uchumi wa Dunia.

**Mheshimiwa Spika,** pia, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu Mheshimiwa Jamal Kassim Ali kwa uweledi wake uliomfanya aweze kuteuliwa tena kuwa Waziri katika Wizara hii mpya pamoja na kuwapongeza watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu ndugu Masoud Hussein Iddi kwa mashirikiano yake anayotupatia wakati wa shughuli za Kamati. Sambamba na hilo, Kamati inamshukuru Katibu Mkuu aliepangiwa kazi nyengine Ndugu Mussa Ali Haji kwa ushirikiano aliotupa alipokuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii, tunamuombea kila la kheri katika majukumu yake mapya.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa umoja wao na uwezo wao, kwa hakika ni Wajumbe mahiri sana. Pia, wameweza kujadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali ambayo yametolewa ufafanuzi na wizara kwa lengo la kuhakikisha kwamba utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa ndani ya ripoti na wakati wa ziara za Kamati kwa Taasisi zilizochini ya Wizara hii; majibu yake ni sahihi na yanauhalisia katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima naomba sasa uniruhusu kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati kwa kutumia Kanuni ya 107(3) inapewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia. Ambapo kazi hii ilifanywa vyema kwa kipindi hiki kilichopita na bado Kamati inazidi kufuatilia utekelezaji wa maagizo hayo kila inapoona inafaa kufanya.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, kwa mujibu wa kanuni ya *109(15)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar,Toleo la 2020. imetoa fursa ya lazima kwa kila Kamati kutayarisha ripoti ya mwaka itakayowasilishwa katika kikao cha mwezi wa Februari cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kanuni ya *109(17)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa maagizo hayo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika kujadili utekelezaji huo.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inaelezea utekelezaji wa maagizo kwa Ofisi ya Rais, Ikulu. Na kama tunavyofahamu kwamba Ofisi ya Rais, Ikulu imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, kifungu cha 50(4). Ofisi hii katika kusimamia na kutekeleza Bajeti yake, ina jumla ya Mafungu *mawili (2)* ambayo ni **Fungu *A 01*** – Afisi ya Rais Ikulu na **Fungu *A 02*** – Baraza la Mapinduzi.

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kwamba Wizara hii ilikua sehemu ndani ya Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, hivyo wakati Kamati inatayarisha ripoti yake kwa mwaka 2021/2022 bado taarifa za Taasisi zilionekana ndani ya Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora na taarifa nyengine zilipatikana Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji. Hivyo, baadhi ya maoni na ushauri wake uligusa Ofisi Kuu hizi mbili kwa kupatiwa usimamizi zaidi wa kisera.

**Utekelezaji wa Maagizo**

**Mheshimiwa Spika,** kiujumla Kamati yetu imeridhishwa sana na utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa kupitia ripoti hiyo isipokuwa kwasasa Taasisi hii inajitegemea, hivyo ni vyema wakazidisha juhudi katika usimamizi na ufuatiliaji wa programu zote zinazotekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 na kuhakikisha kila mmoja anawajibika kwa namna alivyopangiwa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** katika programu zote sita zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais Ikulu, Kamati imetoa ushauri wake kwa kila programu ndogo na hivyo kufanya jumla ya hoja saba ambazo ziliibuliwa na Kamati kuchukuliwa na kufanyiwa kazi. Kwa mnasaba huu, ni kwamba hoja zote zimepatiwa ufafanuzi wa kina na yapo mambo ambayo Kamati imeona ni vyema kuzidi kutiliwa nguvu ili kupata maendeleo endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** katika programu ndogo ya Kuratibu Shughuli za Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi ambayo inasimamiwa na Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi, Kamati inashauri kuwekwa utaratibu mzuri wa wananchi wetu kutuma na kupokea fedha zinazotoka nje ya nchi kwa kupitia benki zetu za Zanzibar badala ya kutumia sehemu zisizorasmi kwa kutuma na kupokea fedha za kigeni kwani njia hii haifaidishi Serikali wala uchumi wetu kama ilivyo kwa nchi za wenzetu ambao wamepiga hatua kubwa kupitia raia wao wanaoishi nje ya nchi kwa kutumia benki zao kwa miamala yote ya kifedha.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati inashauri Wizara kusimamia kikamilifu nafasi ya Zanzibar kushiriki katika mikutano, makongamano na warsha zote za Kikanda ambazo huandaliwa kila mwaka. Vile vile ni vyema nafasi hizi kutumiliwa kwa kupelekwa maafisa wenye uwezo na weledi wa kutosha katika masuala ya ushirikiano wa Kimataifa ili wakirudi kuwe na msaada kwa Serikali yetu na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu katika kujali na kuthamini juhudi za viongozi wetu

ambao hutumia muda wao wote kwa ajili ya maslahi ya umma kwa muda wote wanapokuwa madarakani, Kamati inaishauri Serikali kuiangalia upya “The Political Leaders Retirement Benefits Act, (Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa) Sheria Nam. 6 ya 2006 ambayo pia ilifanyiwa marekebisho kwa baadhi ya vifungu mwaka 2012 ikijulikana kama Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa” Nam. 2 inayolinda maslahi ya viongozi hawa ikiwemo mishahara, maposho na stahiki mbali mbali kwa mujibu wa sheria hii, kwani ni muda mrefu sasa jambo hili halijawahi kufanyiwa maboresho licha ya madiliko ya kiuchumi yanayotokea siku hadi siku na kupanda kwa gharama za maisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu Kamati imeshauri kulitilia nguvu suala la uhifadhi wa nyaraka kwa kukusanya nyaraka muhimu tu na kuzihifadhi sambamba na kutafuta njia maalumu za kujenga ghala za kuhifadhia nyaraka zilizobakia “Strong Room”, hali ambayo itasaidia kuondosha tatizo la ukosefu wa nafasi za kuhifadhia nyaraka hizo. Aidha, Kamati imetilia mkazo suala la kupatiwa mafunzo watendaji wa ofisi hiyo juu ya namna bora ya uhifadhi wa nyaraka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuhitimisha hotuba yangu, naomba shukrani za pekee ziende kwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa namna alivyoleta na kusimamia miradi ya UVIKO 19 ambayo imeanza kuwasaidia wananchi wetu kujikwamua kiuchumi na kijamii. Ushauri wetu ni kuwaomba waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuisimamia kikamilifu miradi hii na kuhakikisha tunaiunga mkono katika utekelezaji wake kwa lengo la kutimiza azma ya Serikali kwenye kuwatumikia wananchi wake. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutosita kuwachukulia hatua wale wote wenye nia mbovu ya kurudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu kwa kuendeleza mianya ya rushwa na uhujumu uchumi katika fedha za umma kwani rushwa ni adui wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kuchukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni machache sana ya Kamati yangu, kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ***Naomba Kuwasilisha.***

Ahsante,

…………………………………

(Machano Othman Said)

***Mwenyekiti,***

***Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,***

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR